**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

*Unapojibu tafadhali taja*

**Kumb.Na. SDC/M.20/10C/32** **Tarehe : 26/06/2025.**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti anawatangazia tena nafasi ya kazi ya **Mjumbe wa Bodi ya Afya Halmashauri** na **Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Hospitali ya Wilaya**, ambayo ilitangazwa tarehe **26.05.2025** kwa tangazo lenye **Kumb.Na.SDC/M.20/10C/23**, wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapo chini mnakaribishwa.

1. **MJUMBE WA BODI YA AFYA YA HALMASHAURI- NAFASI NNE (04)**

   **(a) SIFA ZA WAOMBAJI: -**

   - Awe mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV), Kidato cha sita (VI) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

   **(b) KAZI NA MAJUKUMU YA MJUMBE WA BODI YA AFYA YA HALMASHAURI**

   - Kuhakikisha jamii inapata huduma bora, wanazozimudu na zinazoimarisha afya zao
   - Kuhakikisha upatikanaji na matumizi bora ya rasilimali; fedha, dawa, watumishi na vifaa.
   - Kujadili mipango ya vituo na taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo
   - Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Afya na kufanya ufuatiliaji.
   - Kuwasilisha mrejesho kwa jamii.

2. **MJUMBE WA KAMATI YA USIMAMIZI YA HOSPITALI YA WILAYA - NAFASI TATU (03)**

   **(a) SIFA ZA WAOMBAJI :-**

   - Awe mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV), Kidato cha sita (VI) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**(b) KAZI NA MAJUKUMU YA MJUMBE WA KAMATI YA USIMAMIZI YA HOSPITALI YA WILAYA.**

- Kusaidia kituo katika kupanga na kusimamia masuala ya afya ya jamii
- Kuhakikisha jamii inapata huduma bora, wanazozimudu na zinazoimarisha afya zao
- Kuhakikisha upatikanaji na matumizi bora ya rasilimali; fedha, dawa, watumishi na vifaa.
  - Kubuni vyanzo vya mapato kwa ajili ya huduma za afya
  - Kuhamasisha jamii kuchangia Mfuko wa Afya ya Jamii
- Kujadili mipango ya vituo na taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo
- Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Afya na kufanya ufuatiliaji.
- Kuwasilisha mrejesho kwa jamii

**3. MASHARTI YA JUMLA.**

- Waombaji wote wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 65
- Waombaji wote wawe raia wa Tanzania
- Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu na majina mawili ya wadhamini.
- Waombaji wote waambatishe picha picha mbili za "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma
- Waombaji wote wawe na kitambulisho cha NIDA au namba za kitambulisho
- Maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya Serengeti.
- Waombaji wote wawe ni wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) au NHIF.
- Waombaji waliotuma maombi awali hawapaswi kutuma tena maombi.
- Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 04.07.2025 .**

**Maombi yatumwe kwa Anuani ifuatayo ;**

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti,
S.L.P 176,
**SERENGETI.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI
S.L.P 176
MUGUMU / SERENGETI

Charles V. Rutonesha
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI(W)**